#OKOAMOMBASA

MUHURI Utetezi Wa Haki

MUHURI
MUSLIMS FOR HUMAN RIGHTS

# COVID-19 & OLD TOWN MOMBASA

## Athari ya kufungwa kwa mtaa kwa wanadamu

Nchi ya Kenya ilipata taarifa ya kwanza ya maambukizi Covid-19 tarehe 12 Machi, 2020 Tangu tarehe hii visa vya maambukizi ya Covid 19 vimezidi kuongezeka.

Katika siku za mwanzo wa janga hili la maambukizi Wizara ya Afya ilitambua mitaa ya Eastleigh, Nairobi na Old Town Mombasa kama maeneo yaliyo athirika zaidi na maradhi haya na kuongoza kwa maambukizi. Tarehe 6th Mei, 2020 serikali kuu ilipiga marufuku kuingia na kutoka kwa siku 15 mitaa hii miwili. Amri hii iliongezeka mda na baadae kuondelewa tarehe 6 Juni, 2020

Serikali haikutoa ithibati wala ushahidi wowote wa kuwa mitaa hii miwili ilikuwa imeathirika zaidi na Covid 19 na hivyo kufanya serikali ifunge matembezi aina yoyote mitaa hii. Zaidi ya hapo serikali pia haikueleza sababu ya kuondoa amri ya kuzuwiya matembezi mitaa hii miwili. Zaidi ni kuwa wakazi wa Old Town hawakushauriwa lolote katika kufikiya uamuzi huu wakupiga marufuku kuingia au kutoka. Amri hii ilionekana kama hatua kali sana na wakazi ambao walidhani kuwa ni maonevu ya kisiasa kwa wakazi wa Old Town.

Kufuatia ombi la wakazi wa Old Town, Okoa Mombasa na MUHURI waliandaa zoezi la kutathimini athari ya kufungwa kwa matembezi eneo la Old Town na hususan kujikimu kwa mahitaji ya kimsingi. Kwa zaidi ya siku nne mwezi wa Mei, 2020, vijana 30 kutoka Old Town, walizunguka kuwahoji wakazi. Karibu jawabu 1015 zilipokelewa za mahojiano. Maelezo yaliyomo humu ni mukhtasari wa majibu yaliyopokelewa.

## NAMBARI MUHIMU

**4**
Siku zilizotumika kuwahoji wakazi Juni 2020

**30**
Vijana walo jitolea kueneza makaratasi ya masuala

**32**
Siku mtaa wa Old Town, Mombasa ulifungwa mwezi wa Mei na Juni 2020


**1,015**
Wakazi waliyojibu masuali yaliyo ulizwa

**22,597**
Visa vya maambukizi Covid-19 nchini Kenya kufikia tarehe 4 Agasti, 2020

## Matokeo muhimu:Jee Mna amini kama Covid 19 ipo kweli?

Ili kujuwa kama wakazi wa Old Town walifikiri au kuamini kama janga la Covid 19 lipo, tuliwahoji watu kama walidhani kama Covid 19 ni maradhi yapo kweli na yangeweza kuwa athiri wao.

Zaidi ya nusu (58.6%) ya waliohojiwa hawa amini kuwa janga la Corona lipo kweli. Asilimia 41.3% waliamini kuwa Corona ipo na wengi wao hawa amini kuwa kirusi hichi kiko Africa,au Kenya au Old Town. Baadhi ya waliojibu walihisi kuwa athari na kuweko kwa kirusi cha Corona kumekuzwa kuliko hali halisi ilivyo Kenya. Wachache ya wale waliokuwa na habari kuhusu Corona walikubali kuwa inaweza kuwa athiri na hivyo kukubali kutii maelezo ya serikali,wengine walitowa mifano ya maambukizi katika sehemu zenye misongamano ya watu, kugusana na mtu aliyeathirika, kupeana mikono na tabia za kutojali au kutozingatia usafi.



**58.6%** Hawaamini kuwa Covid ipo kweli


**41.3%** Wana amini kuwa Covid ipo kweli

## Matokeo muhimu:Ukamilifu wa vipimo

Asilimia 95.5% ya wahojiwa 987 hawajawahi kupimwa virusi vya Corona-pengine hali hii haishangazi na inatokana na dhana iliyoko kuwa kirusi hichi si cha kweli. Licha ya hali hii hata wale wanaoamini kuwa kirusi kiko pia hawaja pimwa.

Wengine kati ya walio hojiwa hawamjui mtu aliyewahi kupimwa Covid 19 mtaa wa Old Town. Licha ya hivyo 8.5% hawajui mtu aliyepimwa akapatikana na Covid 19. Kwa jumla watu 953 walohojiwa (96%) hawana habari za mtu yeyote aliyefariki kwa Covid 19.

Sababu kuu waliyotoa wahojiwa kutokwenda kupimwa Covid-19 ilikuwa kuogopa kufungiwa katika vituo ambavyo viwango vyake vya usafi ni duni na wanao pelekwa kutozwa malipo katika vituo hivyo. Mpango huu ulionekana kuzidisha gharama kwa wahojiwa.



**95.5%** Hawajapimwa Covid

**4.5%** Wamepimwa Covid

## Matokeo muhimu:Kupatikana kwa huduma muhimu

Jumla ya wahojiwa 831(82.3% ) walipata msaada wa chakula ulio sambazwa na serikali ya kaunti pamoja na mashirika mengine ilihali 17% (171) walipokea msaada wa pesa taslimu.Kati yao walikuwepo wachache walipokea msaada wa chakula na msaada wa pesa taslimu

Asilimia 74% ya walio hojiwa walipata huduma ya maji safi na usafi, kwa sehemu nyingi huduma hizi zilikuwa bora kuliko siku zilo tangulia kabla ya amri ya kufungwa Old Town. (Ingawa wengine walieleza kuwa huduma ya kupata maji safi na miundo mingi ilikua hali duni zaidi baada ya kufungiwa).

Kupata huduma za Afya zisizohusiana na Covid 19 hazikuwa nyingi. Ni watu 274 (31.5%) ya waliohojiwa walihisi kuwa wameweza kupata huduma hizi za vituo vya Afya kwa maradhi mengine. Pingamizi zilofikiriwa ni pamoja na kupimwa Covid 19 na kuzuiliwa, ukosefu wa hospitali mtaa wa Old Town,uchache wa maduka ya kuuza madawa. Asilimia 56.5% waliona kuna vigumu kupata soko la maboga freshi. Kununuwa bidhaa madukani kulionekana rahisi.

**82.3%** Walipata msaada wa chakula

**17%** Walipata msaada wa pesa taslimu

**74%** Waliapata maji na huduma ya usafi

**56.5%** Walihisi ugumu kupata mboga

**31.5%** Walio hisi kutokuweko kwa huduma za afya zisizo husika Covid

## MAPENDEKEZO

Wakazi wa old town walitoa mapendekezo yafuatayo:

- Serikali ya kaunti itoe sababu zilizo zizingatia na kufikia amri ya kuufunga mtaa na kuzuwia watu kutoka au kuingia;
- Kuwalipa gharama wale waliotozwa pesa katika vituo walivyo pelekwa karantini. Hii ni kutokana na ahadi serikali iliyotoa kuwa watu walio wekwa karantini watalipiwa;
- Ridhaa kutoka idara za seriakli kutoka na madhial waliyopitia yakiwemo hasara za biashara wakati wa ramadhan,ukosefu wa mapato na huduma muhimu na amri ya kutotembea isiyo ya dharura na kutoweza kuabudu kama dini inavyopasa;
- Ridhaa kutoka kwa viongozi wa siasa kwa kutumia vitisho ,mabavu na kukosa kuwa kuhusisha umma kabla ya kutangaza amri ya kutotoka inje.

## LOCKDOWN OR SHAKEDOWN?

**94%**

Ya wahojiwa walieleza "ugumu" wa walio pata kutoka Old Town ilipo tolewa ya amri ya kufungiwa

**20 KES**

Hongo ulo hitajika kulipa ili kutoka Old Town siku za kufunguwa